

HALMASHAURI YA WILAYA YA SINGIDA



TANGAZO


MFUMO WA VIBALI VYA KUSAFIRI NJE YA NCHI

Mfumo wa vibali vya kusafiri ni mfumo wa kimtandao unaojiendesha wenyewe (otomati) uliotengenezwa kwa ajili ya Serikali ya Jamhuri wa Muungano wa Tanzania.

Kwa kutumia mfumo huu waajiriwa wa Serikali na watumishi wote wa umma wanaweza kuomba kibali cha kusafiri nje ya nchi kwa safari binafsi au za kikazi kwa mtu binafsi au kikundi kwa njia ya mtandao.

Hivyo mtumishi yeyote mwenye mpango wa kusafiri nje ya nchi awasiliane na kitengo cha TEHAMA na Uhusiano kwa maelezo na msaada zaidi juu ya namna ya kuweza kutumia mfumo huu.

Imetolewa na:


Steven A. Kasanga,
Kitengo cha TEHAMA na Uhusiano,
Halmashauri ya Wilaya,
SINGIDA.

10 Mei 2018